# SWALA YA JAMAA
# NI KIELELEZO CHA UMOJA
# NA MSHIKAMANO
# صلاة الجماعة بحث فقهي اجتماعي


**Kimeandikwa na:**
**Sheikh Hasan Musa As- Safar**

الشيخ حسن الصفار

**Kimetarjumiwa na:**
**Abdul – Karim Juma Nkusui**

**Kimehaririwa na:**
**Hemedi Lubumba (Abu Batul)**


Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe. Ewe Mwenyezi Mungu mteremshie rehema Muhammad na Kizazi cha Muhammad, kama ulivyomteremshia Ibrahim na Kizazi cha Ibrahim, na umbariki Muhammad na Kizazi cha Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na Kizazi cha Ibrahim.

## UTANGULIZI

Mwenye kusoma sira ya Maimamu wa Ahlul – Bait (as) na kutafakari kauli zao na wasia wao atafahamu upeo wa kujali kwao umoja wa umma na kutilia kwao maanani hali ya kuunganisha safu zao na kuepusha mfarakano na mgawanyiko baina yao. Wao hawakuingia katika kinyang'anyiro cha madaraka na usultani licha ya kwamba walikuwa na yakini kwamba ukhalifa ni haki yao, na licha ya kwamba wafuasi wao waliamini na wataendelea kuamini ubora wao na uwezo wao.

Pia Maimam walitoa kila kilicho katika uwezo wao kwa ajili ya kuupa nguvu umma pamoja na kuwasaidia Makhalifa na watawala katika kuziba mianya na mapengo kwa kutoa rai na ushauri, kutoa nasaha na maelekezo. Maimam waliwalea wanafunzi wao na wafuasi wao kujali maslahi makuu ya Uislamu na umma, na kuweka maslahi binafsi nyuma ya maslahi ya Uislamu na umma. Wamewausia wafuasi wao kujiingiza ndani ya umma na kupiga vita kila jaribio la kutengwa na kubaguliwa kutoka kwa wakandamizaji na madhalimu.

Ni kweli kwamba madhehebu ya Ahlul-Baiti (as) yana mtazamo wake mahususi wa kifikra na kifiqihi, lakini hiyo haimaanishi kwamba wafuasi wao wakubali hali ya kujibagua na kujitenga mbali na umma. Siasa ya kujumuika pamoja, umoja na mshikamano ambayo waliizatiti Maimam wa Ahlul- Bait (a.s.) imeleta faida bora, kubwa. Ni faida kwa maslahi ya umma wa Kiislamu na kwa maslahi ya Ahlul-Bait (a.s.), faida hiyo ni:-

**Kwanza:** Imehifadhi umoja wa umma na kuzuia kwa kiasi kikubwa mfarakano wa kimadhehebu katika zama zote.

**Pili:** Imewapotezea maadui na wakandamizaji fursa nyingi ya kuushughulisha umma na hitilafu za kimadhehebu.

**Tatu:** Imetoa fursa ya kutanuka kwa madhehebu ya Ahlul-Bait na wigo wake kukua ndani ya umma.

Na kati ya kielelezo cha mfumo huu wa umoja na siasa yenye hekima ya Maimam ni rai yao na msimamamo wao katika kushiriki swala ya jamaa ya Waislam licha ya kuwepo ikhitilafu za kiitikadi na za kifiqihi, na licha ya kuwepo matatizo na mibinyo ya kisiasa ambayo ilikuwa ikiwazunguka wao na wafuasi wao.

Uchambuzi huu mchache uliopo mbele yako msomaji mtukufu ni maelezo na uthibitisho wa msimamo huo wa kisharia wa umoja huo, nimeona kuna umuhimu niutoe ili kuwakumbusha Shia wa Ahlul-Bait (a.s.) na wafuasi wao juu ya maelekezo ya Maimamu wao waongofu (as) na kutoa sura ya mwelekeo wenye nuru wa sira ya Ahlul-Bait (a.s.) na nyumba ya utume (as).

Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu ayajaalie haya yawe ni kwa ajili ya kutaka radhi Zake, na yawe ni mchango katika kueneza utamaduni wa uelewano kuelekea katika umoja na ushirikiano, na shukrani zote njema ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu.

Hasan Musa As-Safari.
4 Jumadul- Akhir 1429 A.H/ 8 Januar 2008.

## SWALA YA JAMAA NA TOFAUTI ZA KIMADHEHEBU

Kuna aina mbili za ikhtilafu na ijtihadi baina ya madhehebu za Kiislam, nazo ni ikhtilafu za kifiqhi na ikhtilafu za kiitikadi, na kila madhehebu ina hoja zake na dalili zake katika mwelekeo wake wa kifiqhi na kiitikadi. Na zote ni za zamani zimekuwa pamoja na historia ya umma, na humo kuna chimbuko la mengi kati ya athari za kisiasa na kijamii katika uhusiano wa ndani baina ya umma. Na kati ya sehemu ambazo zimeathirika kutokana na ikhtilafu hizo za kifiqhi na kiitikadi ni swala ya jamaa, ambayo Mwenyezi Mungu ameitaka iwe ni udhihirisho wa mkusanyiko wa Waislamu na umoja wao. Ambapo maimamu wa medhehebu wametafiti mas'ala yenye kuafikiana na yenye kutofautiana ya kimadhehebu baina ya maamuma na imam katika nyanja za kifiqhi na za kiitikadi.

### Tofauti za Kifiqhi:

Maulanaa wa Kisunni na wa Kishia wameafikiana kwamba sio sharti kuafikiana baina ya imam na maamuma katika mas'ala mengine ya kifiqhi isipokuwa yale yanayofungamana na swala ya imam mwenyewe. Hivyo inasihi kumfuata imam anayetimiza sharti za imam wa jamaa hata kama atatofautina na maamuma katika ijtihadi au taqlid katika mas'ala mengine ya kifiqhi. Ama ikiwa tofauti ya kifiqhi baina ya maamuma na imam inahusu jinsi imam anavyotekeleza swala yake, basi jopo la maulamaa kutoka katika Sunni na Shia wameweka sharti kwamba, swala ya imam ni sharti iwe sahihi katika madhehebu ya maamuma na katika maoni yake, katika ijtihadi yake na taqlidi yake.

Maulamaa wa Shia wamesema: Tegemeo katika nyanja zote ni kwamba swala ya imam kwa uhakikia wake iwe sahihi kwa mtazamo wa maamuma. Hivyo haijuzu kumfuata ambaye swala yake ni batili kwa mtazamo wa maamuma utokanao na ijtihadi au taqlid. Katika hali isiyokuwa hiyo inajuzu kumfuata.

Hayo pia yamesemwa na Mahanafi na Mashafii ambapo wameona kwamba kati ya sharti la imam ni kwamba swala yake iwe sahihi kwa mujibu wa madhehebu ya maamuma, lau Hanafiy akiswali nyuma ya Shafii na akatokwa na damu na wala asitawadhe baada yake, au Shafii akiswali nyuma ya Hanafi aliyemgusa mwanamke mathalan, basi swala ya maamuma ni batili, kwani kwa mtazamo wa kila mmoja swala ya imam wake ni batili kwa itifaki ya Hanafii na Shafii.[1]

Mahanafi wanasema: Inachukiza kuswali nyuma ya Shafii. Na Mashafii wanasema ni bora kuswali nyuma ya imam wa Kishafii na sio wa Kihanafi wala mwinginewe.[2]

Na Mamaliki na Mahambali wamekhalifu ambapo wamesema: Kilicho sharti na cha kuzingatiwa katika kusihi swala ni madhehebu ya imam tu, nayo ni kwamba swala yake

---

[1] *Minhaajus-Swalihiyna* Juz. 1 mas'ala 81, chapa I, ya mwaka 1423 A.H cha Sayyid Sistaniy- Qum

[2] *Alfiqhul-Islamiy wa Adilatihi* cha Azahiyli, Juz. 2, Uk. 181, chapa 3 ya mwaka 1409 A.H. Chapa ya Darulul-Fikri- Damascus.

iwe sahihi kulingana na rai ya madhehebu yake na sio kulingana na madhehebu ya maamuma.

Kama Malikiy au Hambaliy atamfuata Hanafii au Shafii na ikawa hakupaka kichwa chake chote katika udhu, basi swala yake ni sahihi, kwa kuwa swala ya imamu kwa mujibu wa madhehebu yake ni sahihi. Ama yaliyo sharti katika kusihi kufuata, mazingatio humo ni madhehebu ya maamuma, hivyo Malikiy au Hambaliy anayeswali faradhi akimfuata Shafii anayeswali sunna basi swala yake ni batili kwa sababu sharti la kufuata ni kuafikiana swala ya imam na maamuma.[1]

Mazaidia wameafiki rai ya Mamaliki na Mahambali, wakasema: Watu wawili wakitofautiana katika madhehebu katika mas'ala ya ijtihadi, mfano mmoja wao anaona kwamba kusema amin katika swala ni sheria, na mwingine akaona kwamba inaharibu swala, au kutoka damu kunatengua udhu na mwingine akaona kuwa hakutengui, au mengine mfano wa hayo, hapo imam ndio mwamuzi, hivyo inasihi kila mmoja kumswalisha mwenzake, kwa sababu kama tukisema kinyume cha haya inasababisha watu kujizuia kuwaswalisha baadhi yao katika hali nyingi, na kujizuia kwenda katika misikiti yao, na haya hayakujitokeza kwa masahaba licha ya kuwepo tofauti baina yao[2].

## Tofauti ya kiitikadi:

Misingi ya itikadi inaafikiwa na Waislamu wote nayo ni ile iliyotajwa na Qur'ani Tukufu, kuanzia na kumwamini Mwenyezi Mungu, Mitume wake, vitabu vyake, malaika wake na Siku ya Mwisho. Lakini tofauti imetokea baina ya Maulamaa wa umma juu ya ufafanuzi wa misingi hiyo katika yale yanayohusiana na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, sira ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na tafsiri ya aya za Qur'ani, na mfano wa hayo.

Na tofauti hii ya kiitikadi ni kubwa na pana kuliko tofauti ya kifiqhi, hususani kila upande unapolazimisha upande mwingine kwa kauli ambazo hauzisemi, na wakati mwingine kumetokea baadhi pande kuutuhumu upande mwingine katika dini yake, kama vile kumwita mushriku au mwanabidaa. Hayo yameakisi pia katika mtazamo wa fiqhi kwa yale yanayoambatana na uhusiano wa ndani baina ya wanajamii, na kati ya sehemu zilizo wazi zaidi ni imam wa jamaa, ambapo wengi wa maimam wa madhehebu wameweka sharti katika kusihi uimamu wa jamaa kuwa ni kutotofautiana itikadi katika mambo ya msingi ya kila madhehebu.

---

[1] Al-Jaziriy: Sheikh Abdur-Rahman katika *Fiqhul-Islamiy alaa madhahibiI- Ariba'a* Juz. 1 Uk. 366, chapa ya Darul-Ihyai Turathil-Arabiy- Beirut.
[2] Al –Anasiy As-Swanaaniy: al -Alammah Ahmad Qasim katika *Tarikhul–Madhahibil-Arba'ah* Juz. 1, Uk. 112. Maktabatul-Yamanil-Kubraa - Sanaa.

Baadhi ya maimam wametofautisha baina ya yule anayedhihirisha na kulingania bidaa yake, huyo haisihi kuswali nyuma yake, na baina ya yule asiyedhihirisha wala halinganii, huyo inasihi kuswali nyuma yake.

Ibnu Qudamah amesema: Mwenye kumfuata imam mwenye kudhihirisha bidaa na kuitangaza, kulingania au kujadiliana juu yake, basi ni juu yake kuirudia, ama asiyedhihirisha bidaa yake, hakuna kurudia kwa mwenye kumfuata hata kama anayaitakidi hayo.

Al-Aritham amesema: Nilimuuliza Abu Abdillahi Imam Ahmad bin Hambal: "Unasemaje kuhusu Marawafidh wanaotangaza?" Akasema: "Ndio namwamuru arudie swala." Akaambiwa: "Ndivyo hivyo kwa kila mwanabidaa?" Akasema: "Hapana, hakika kati yao kuna wanaonyamaza na kuna wengine wanaokoma na wala hawazungumzi."

Na akasema: "Usiswali nyuma ya yeyote kati ya watu wa matamanio ikiwa atakuwa analigania matamanio yake."

Na amesema: "Usiswali nyuma ya Murjiu ikiwa atakuwa analingania."

Na imepokewa kutoka kwa Ahmad kwamba: "Hakuna kuswali nyuma ya wanabidaa kwa hali yeyote ile."

Amesema katika riwaya ya Abil-Harith: "Hakuna kuswali nyuma ya Murjiu na Rafidhi, wala fasiki, isipokuwa kama atawaogopa basi ataswali na atairudia."

Abu Daud amesema: Ahmad amesema: "Utakaposwali nyuma ya mwenye kusema kwamba Qur'ani imeumbwa basi uirudie."

Na kutoka kwa Maliki: "Hakika hakuna kuswali nyuma ya wanabidaa."

Natija ni kwamba mweye kuswali nyuma ya mwanabidaa mwenye kudhihirisha bidaa yake, ni juu yake kuirudia. Na kwa asiyedhihirisha, kuirudia kwake kuna riwaya mbili:

Al-Hasan, Abu Ja'far na Shafii wameruhusu kuswali nyuma ya wanabidaa. Na amesema Ibnu Mundhir na baadhi ya Shafii: "Ambaye tunamkufurisha kwa bidaa yake, swala haiswaliwi nyuma yake. Na kwa yule tusiyemkufurisha inasihi kuswali nyuma yake."[1]

Maulamaa wa Kishia wameafikiana juu ya sharti la imani katika kusihi uimam wa jamaa, kwa maana ya kwamba aamini Uimam wa Maimamu kumi na wawili wa Ahlul- Bait(as), na kwamba haisihi kufuata jamaa kwa asiye kuwa hivyo.

---

[1] Ibnu Qudaamah: Abdillahi bin Ahmad katika *Al- Mughuniy* Juz. 3, Uk. 17- 18 chapa I ya mwaka 1412 A.H Kilichotolewa na Hijir - Cairo.

## KUSWALI JAMAA KWA DHARURA

Mwanadamu ni lazima ajifunge kwa kanuni na hukmu za kisheria katika kutekeleza ibada zake na mafunzo yake ya kidini. Kanuni hizo na hukumu zinaelezea maoni ya sheria kulingana na ijtihadi ya mkalafu au taqlidi yake kwa wanachuoni wa madhehebu anayoyafuata na kuitakidi usahihi wake. Na panapokuwa na masharti yaliyokubaliwa katika kusihi uimam wa jamaa basi mukalafu haisihi kwake kumfuata katika swala yake imam asiyetimiza masharti hayo, kwa sababu swala yake itakuwa batili na wajibu wake utabakia pale pale ukimtaka autekeleze.

Lakini akilazimika katika hilo kwa kuogopa nguvu za imamu wa jamaa ambaye hatimizi masharti ya kusihi uimamu wake au kwa kuogopa adha ya wafuasi wake na jamaa zake, hapa kuna kanuni za kisharia zilizo wazi kama vile kauli yake (swt): **"Isipokuwa mwenye kulazimishwa hali ya kuwa moyo wake umetulizana kwa imani." (Sura an-Nahli: 106)**. Na kauli yake: **"Isipokuwa mkiogopa madhara kutoka kwao." (Sura Aal Imran: 28)**. Na kauli yake: **"Na hakujaalia uzito kwenu katika dini." (Sura al-Haj: 78)**. Na nyinginezo kati ya nususi za kidini.

Wakati huo inajuzu kwa mukalafu kuswali jamaa ambayo imamu wake hana sifa zilizokubaliwa katika kusihi uimamu. Na haya ni ambayo Maulamaa wa umma wameafikiana juu yake pamoja na kuhitalifiana madhehebu yao, lakini wao wametofautiana je swala hiyo yatosheleza kwa njia ya taqiya na dharura au ni juu yake kuirudia?

Imekuja katika *Al-Mughuniy* ya Ibnu Qudamah katika riwaya ya Abi Harith – kutoka kwa Ahmad bin Hanbali: "Haiswaliwi nyuma ya Murjiu, Rafidh wala fasiki isipokuwa akiwaogopa, basi ataswali kisha atairejea."

Pia imekuja humo: "Ibnu Umar alikuwa anaswali nyuma ya Al-Hajaj. Na Hasan na Husein (a.s.) na wengineo katika masahaba walikuwa wanaswali pamoja na Mar'wan. Na wale ambao walikuwa katika utawala wa Ziyadi na mtoto wake walikuwa wanaswali pamoja nao. Na waliswali nyuma ya Walid bin Uqbah, na tayari alikuwa alishakunywa pombe na kuwaswalisha swala ya asubuhi rakaa nne, kisha akawaambia: Niwaongezee? Hivyo hii ikawa ni kongamano….. na kitendo hiki cha Masahaba kinachukuliwa kuwa waliogopa madhara kwa kuacha kuswali pamoja nao."[1]

Maulamaa wa Kishia wametoa fatwa ya kujuzu swala nyuma ya imamu asiyetimiza masharti ya kusihi uimam kwa taqiya au kuogopa madhara, na kwamba inatosheleza swala yake ya wajibu na wala hakuna haja ya kuirudia, kwa sharti asome mwenyewe.

[1] *Al-Mughuniy* ya Ibnu Qudamaah Juz.: 3, Uk. 20 – 21.

## SWALA YA JAMAA KWA KULETA UKURUBA

Wafuasi wa Madhehebu kwa kufuata rai ya Maimamu wao (a.s.), imamu wao katika swala ya jamaa huwa ni yule anayetimiza masharti ya kusihi uimam, na kati ya hayo ni kuafikiana au kutotofautiana kiitikadi katika vipengele vya msingi ambavyo madhehebu yametofautiana kwavyo.

Na hayo ndiyo yaliyopo hasa katika jamii ya Kiislam kwa Sunni na Shia, ambapo maimamu wa miskiti na jamaa katika kila kaumu huwa yule aalimu na mlinganiaji ambaye ni wa ndani ya madhehebu yao na si wa nje ya madhehebu yao, hususan imam wa jamaa aliyeratibiwa ambaye huwa ni chanzo cha kuelekeza na kufundisha dini. Wanachukua kwao hukumu zao za kisheria na wanarejea kwao katika mambo yao ya kidini. Hivyo ni lazima awe ni msemaji wa madhehebu anayoyafuta. Na katika nchi ambazo humo kuna madhehebu mengi ya kiitikadi kama vile Shia na Sunni kila wafuasi wa madhehebu huwa na miskiti yao maalum kulingana na ikhtilafu zao katika baadhi ya matawi ya hukumu za swala, nalo ni jambo la kawaida na ni haki ya kisharia itokanayo na hali ya kuheshimu mitazamo ya kimadhehebu ambayo hutengeneza hali za kidini ambazo ni wajibu kuzifuata kama mwanamadhehebu, kwa kila upande.

Hali hiyo haipingani na msingi wa Umoja wa Kiislam, umoja hauzuiliwi na wingi wa madhehebu wala haufuti haki ya ijtihadi na kuwepo kwa ikhtilafu ya rai ndani ya wigo wa kuheshimiana baina ya pande zote, na kujali masilahi makuu ya Uislam na umma. Baadhi ya wanaofahamu wanaweza kutamani umoja wa daraja la juu kabisa baina ya Waislam, ule unaovuka na kuondoa vikwazo vya kimadhehebu ndani ya miskiti na katika swala za jamaa, yaani misikiti iwe ya kushirikiana baina ya Sunni na Shia kwa kila mmoja kuswali nyuma ya mwenzake. Hili ni tarajio zuri sana, lakini kulifikia kwake inahitaji rai ya kisheria kutoka kwa maimamu wa madhehebu katika yale yanayohusu masharti ya kusihi kwa uimam wa jamaa kama ilivyotangulia.

Sharia inasema nini iwapo utapatikana mkutano ambao utawafanya Shia wajikute wapo eneno ambalo hapo husaliwa Swala ya jamaa ya Kisunni, au Sunni wajikute wapo eneo ambalo hapo husaliwa Swala ya jamaa ya Kishia, bila kuwepo hofu aina yoyote. adha yoyote wala hatari yoyote toka pande nyingine? Je katika hali hii watatofautiana na kusimamishwa jamaa mbili katika sehemu moja na wakati mmoja? Au wafuasi wa madhehebu nyingine wataondoka katika sehemu hiyo licha ya kwamba Swala ya jamaa imesimamishwa? Au wataswali furada na hali swala ya jamaa inasimamishwa mbele yao?

Hakika hali zote hizi zinapingana na hali ya kijamii na zinaleta msuguano na kinyaa na zinaharibu uelewano na umoja na mandhari ya mshikamano na ukuruba. Hivyo Maimamu wa madhehebu wametoa fatwa kwa wafuasi wao kufuata jamaa inayosimamishwa mahala walipo hata kama ni kwa nia ya kufuata tu na sio kwa nia ya umaamuma hasa, hiyo ni kwa kujali adabu, na kuhifadhi mandhari ya umoja na mshikamano.

Ibnu Qudamah amesema katika *Al –Mughuniy*: "Ikisimamishwa swala na mtu yuko msikitini na imamu ni kati ya wasio sihi kwa uimamu, akitaka ataswali nyuma yake, kisha atairudia. Na kama akinuia furada na akaafikiana na imamu katika rukuu, sajda, kisimamo, kukaa, basi swala yake ni sahihi, kwa sababu ameleta vitendo vya swala na masharti yake kwa njia ya ukamilifu. Hivyo haiharibiki kwa kuafikana kwake na imamu katika vitendo kama hakuwa amekusudia kuafikiana. Na imepokewa kutoka kwa Ahmad kwamba atarudia swala."

Athram amasema: "Nilimwambia Abu Abdillah - Ahmad bin Hanbal - mtu anakuwa msikitini na swala inakimiwa, na mtu huyo hapendi kuswali nyuma ya mtu anayewaswalisha, na ni makruhu kutoka msikitini baada ya adhana kwa mujibu wa kauli ya Nabii (saww), je, atafanyeje?" Akasema: "Kama atatoka huo utakuwa ni uovu, lakini ataswali pamoja naye na kisha atairudia. Na akitaka ataswali swala yake furada, ataswali yeye binafsi, atatoa takibira mwenyewe na kurukuu mwenyewe na atasujudu mwenyewe na wala hatojali sijda yake kuafikiana na sajida ya imam, na takibira yake kuwa pamoja na takbira ya imam."

Maimam wa Ahlul-Bait (as) walikuwa ni viongozi katika kuanzisha msimamo huu wa umoja na wamewahimiza wafuasi wao kushiriki katika swala ya jamaa pamoja na ndugu zao Waislam miongoni mwa Ahlus-Sunna licha ya kuhitalifiana nao kiitikadi na kifiqhi katika ufafanuzi wa wajibati za swala. Na bila kujali ile dhulma na uonevu waliokuwa wakikumbana nao wao wafuasi wa Ahlul-Bait (as).

## KAULI ZA MAIMAMU WA AHLUL-BAIT (A.S.)

Sira ya Ahlul-Bait (as) ilikuwa imesimama juu ya msingi wa kuhifadhi Umoja wa Umma na kuzuia mgawanyiko katika safu zake, kwa ajili hiyo walikuwa wanaamuru wafuasi wao na Shia wao kuhudhuria katika mikusanyiko ya umma na kutojitenga na kujibagua, walikuwa wanahimiza juu ya kuimarisha ushirikiano na kuipa nguvu jamii na wanajamii ili kwamba ikhtilafu za kiitikadi zisiwe ni sababu ya utengano na kudharauliana, na ili kukosekana kwao katika harakati za kijamii kusitowe mwanya wa kuchafuliwaa sifa yao na kubambikiziwa tuhuma mbalimbali.

Ndani ya rejea za Hadithi za Madhehebu ya Alhul-Bait (as) kuna makumi ya nususi na riwaya ambazo zinatilia mkazo kushiriki swala ya jamaa pamoja na Waislamu wengine wanaotofautiana na Shia miongoni mwa Ahlus-Sunna, na kuzihesabu swala hizo kuwa ni kati ya sehemu zenye thawabu bora zaidi, na kwamba malipo ya swala hiyo ya kusali pamoja na Ahlus-Sunna ni mengi mno mbele ya Mwennyezi Mungu. Hakuna tafsiri ya hilo isipokuwa ni kwa kutazama athari nzuri ambazo zinapatikana kutokana na ushirikiano na kudumisha hali ya mawasiliano na uelewano, mshikamano na umoja baina ya wanajamii, na kupoteza kabisa fursa kwa wakandamizaji na wachochezi ambao wanataka kuushughulisha umma kwa ikhitilafu za ndani.

Na ifuatayo ni baadhi ya mifano hiyo:-

Kutoka kwa Jabir Al-Ja'afiy amesema: "Nilimuuliza Abu Ja'far Al-Baqir (as): 'Hakika mimi nina majirani baadhi yao wanajua jambo hili – yaani wanaamini uongozi wa Ahlul-Bait (as) - na baadhi yao hawajui wameniomba niadhini na kuwaswalisha, nikaogopa hilo lisije likawa zito kwangu.' Akasema: 'Adhini, waswalishe na chunga muda.'"[1]

Imekuja katika sanad sahihi kutoka kwa Hamid bin Uthman kutoka kwa Abu Abdillah As-Swadiq (as) kwamba amesema: "Atakayeswali nao katika safu ya kwanza atakuwa kama yule aliyeswali nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) katika safu ya kwanza."[2]

Na kutoka kwa Imam As-Swadiq (as) hakika amesema: "Utakaposwali nao Mwenyezi Mungu atakusamehe kwa idadi ya watakao kuwa nyuma yako."[3]

Kutoka kwa Hasan bin Said kutoka kwa Abu Ali –katika hadith amesema. "Nilimwambia Abu Abdillah: 'Hakika sisi tuna imamu anayetukhalifu, na anawachukia jamaa zetu wote.' Akasema (as): 'Achana na kauli yake. Wallahi kama wewe ni mkweli basi wewe una haki zaidi na msikiti kuliko yeye, basi kuwa wa kwanza kuingia na wa mwisho kutoka, na tabia yako kwa watu iwe nzuri, na sema kauli nzuri."' [4]

Kutoka kwa Is'haq bin Ammar amesema: "Aliniambia Abu Abdillah as-Swadiq (as): 'Ewe Is'haq! Je, unaswali nao msikitini?' Nikasema. Ndio. Akasema: 'Swali pamoja nao hahika anayeswali pamoja nao katika safu ya kwanza ni kama yule anayenyanyua upanga wake katika njia ya Mwenyezi Mungu.'"[5]

Kutoka kwa Abu Abdillah bin Sanan amesema: "Nilimsikia Abu Abdillah (as) anasema: 'Nawausia kumcha Mwenyezi Mungu Mtukufu, msiwabebe watu kwenye mabega yenu mtadhalilika. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Kitabu chake: Na waambieni watu kauli nzuri.' Kisha akasema: Tembeleeni wagonjwa wao, sindikizeni majeneza yao na toeni ushahidi kwao na juu yao, na swalini pamoja nao katika misikiti yao."'[6]

Kutoka kwa Zaid As-Shahaam kutoka kwa Ja'far bin Muhamand (as) hakika alimwambia: "Ewe Zaid! Amiliana na watu kwa tabia zao, swali katika misikiti yao, tembelea wagonjwa wao, shuhudia majeneza yao, na kama mtaweza kuwa maimamu na waadhini basi fanyeni hivyo, kwani mtakapofanya hivyo watasema: Hawa ni wafuasi wa Ja'fari, Mwenyezi Mungu amrehemu Ja'far, ni adabu nzuri ilioje aliyowafunza wafuasi wake. Na kama mtaacha hayo watasema: Hawa ni wafuasi wa Ja'far, ni adabu mbaya ilioje aliyowafunza wafuasi wake."[7]

---

[1] *Al – Mughuniy* ya Ibnu Qudamah Juz. 3, Uk. 25.
[2] *Jamiu Ahaadithis-Shiah* hadith ya 10996, cha Sayyid Huseiniy Tabatabaiy Al-Burjurdy chapa ya 1417- Qum
[3] *Wasailus-Shiah,* Hadith no: 10717 chapa 1 ya mwaka 1993 ya Muasasatu Aal Al-Bait liihiyai Turath - Beirut
[4] *Wasailus-Shiah,* Hadith no: 10717 chapa 1 ya mwaka 1993 ya Muasasatu Aal Al-Bait liihiyai Turath - Beirut
[5] *Wasailus-Shiah,* Hadith no: 10717 chapa 1 ya mwaka 1993 ya Muasasatu Aal Al-Bait liihiyai Turath - Beirut
[6] *Wasailus-Shiah,* Hadith no: 10717 chapa 1 ya mwaka 1993 ya Muasasatu Aal Al-Bait liihiyai Turath - Beirut
[7] *Jamiu Ahadithus-Shiah* Hadith no: 10995 cha Sayyid Huseiniy Tabatabaiy

Kutoka kwa Ali bin Ja'far katika kitabu chake, kutoka kwa kaka yake Musa bin Ja'far (as) amesema: "Hasani na Husein (a.s.) wameswali nyuma ya Mar'wan na sisi tunaswali pamoja nao."[1]

## FATWA ZA MAULAMAA WA KISHIA

Kwa uongofu na maelekezo ya Maimum wa Ahlul-Bait (as), na kwa kuhami Umoja wa Umma, kuhifadhi uelewano na maafikiano baina ya watu wake, Maulamaa wa Kishia wa zamani na sasa wametoa fatwa ya kupendeza ya kuhudhuria swala ya jamaa pamoja na Ahlus-Sunna, na kwamba mwenye kuswali pamoja nao anapata thawabu za jamaa, na swala yake ni sahihi inatosheleza na haihitaji kuirejea.

Shahidi wa kwanza Muhammad bin Makkiy Al-Amily amesema katika *Durusus-Shar'iyah*: "Na ni suna kuhudhuria jamaa ya Kisunni kama ambavyo ni suna kuhudhuria jamaa ya Kishia, bali ni bora kwani imepokewa kwamba: 'Mwenye kuswali pamoja nao katika safu ya kwanza ni kama mwenye kuswali nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww).' Na inatiwa mkazo pamoja na ujirani. Mahala pa kudhihirisha atasoma kwa siri, kimoyo moyo. Na inaporomoka kwake kusoma kama atawakuta katika hali ya rukuu yao, hapo atatimiza (rukuu) kama ikiwezekana, vinginevyo nayo itaporomoka kabisa kwake." [2]

Sayyid Abdul-Husein Sharaf Diyn amesema: "Amirul-Muuminina – Ali (as) amekataa kuswali isipokuwa kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kutekeleza aliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu, na kuswali kwake nyuma yao – yaani Makhalifa – haikuwa ila kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nasi tumemfanya (as) kigezo hivyo tunajikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuswali nyuma ya wengi kati ya maimam wa jamaa ya Ahlus-Sunna hali yakuwa na ikhilasi katika swala hizo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na haya yanajuzu katika madhehebu ya Ahlul-Bait (as), na mwenye kuswali kati yetu nyuma ya imam wa Kisunni analipwa kama ambavyo analipwa kwa kuswali nyuma ya imam wa Kishia. Na mjuzi wa madhehebu yetu anajua kwamba sisi tunaweka sharti la uadilifu wa imam wa jamaa anapokuwa Shia, hivyo haijuzu kumfuata fasiki katika Shia wala kwa asiyejulikana hali yake. Ama kwa Sunni inajuzu kumfuata bila sharti."[3]

Na kama maulamaa wanatafiti mas'ala haya kwa anwani ya taqiya hiyo ni kwa sababu taqiya kwao kama inavyofahamika kutokana na nasi za kidini haitumiki tu kwenye sehemu za hofu juu ya nafsi, mali na utu tu, bali inahusu pia hofu juu ya maslahi ya Uislamu na umma, kwa kujali umoja na uelewano baina ya safu za watu wake, na hiyo ndio nyanja muhimu zaidi na ya msingi katika maudhui.

---

[1] *Jamiu Ahadithus-Shiah* Hadith no: 10725 cha Hurul-Amiliy Muhammad bin Hasan

[2] Al–Aamily Muhammad bin Makiy katika *Durusus- Shar'iat* ndani ya *Silsilatu Yanabi'il Fiqihiyat* Juz. 1, Uk. 651 cha Ali Asghar Mardawiyd, chapa I ya mwaka 1413 A.H, ya Daru turath – Beirut.

[3] Mausuatu ha Imam Sayyid Abdul Husein Sharaf Diyn: Markazil-Ulumi wa thaqaafatil Islamiyah katika *Ajwibatu Masail Musa Jaarallah* Jz: 4, uk: 1427H Darul Muarikhil Arabiy – Beirut.

**Rai ya Sayyid As-Sabzawary:**

Mwanachuoni Sayyid Abdul-A'alaa As-Sabzawary anasema kuhusu taqiya: "Sehemu yake ni pale inapopatikana hofu juu ya nafsi au heshima au mali, sasa hivi au hata baadae au kwa ajili ya upendo na uelewano hata kama hofu si ya dhahiri. Dalili juu ya upana huu ni ujumla wa dalili zinapendekeza hilo, ambapo dhahiri yake ni kuraghibisha hilo, ambazo zinaonyesha kwamba kupatikana upendo na uelewano, na kuondoka hali ya kutoelewana na kukimbiana ni kati ya mambo yanayowajibisha hilo (taqiya), sasa itakuwaje katika sehemu za hofu? Hapana shaka kwamba kuondoa utengano na kupatikana upendo baina ya Waislamu ni suala muhimu zaidi kuliko kuacha kikwazo au sehemu katika amali zisizo za msingi, hiyo ni kutokana na Mtukufu Nabii na Mawasii wake maasumina (a.s.) kujali sana hilo na kulitilia sana maanani, kama ambavyo haifichikani kwa mwenye kurejea maisha yao. Hivyo – taqiya - ni wajibu ama kwa kuwepo madhara na hofu, hiyo ni kwa mujibu wa hoja za jumla, na ama kwa kutokuwepo kwake, lakini kwa ajili ya kupatikana upendo na kuondoa utengano, hiyo ni kwa mujibu wa dalili zilizotangulia zinazoonyesha wajibu wake……… Abu Ja'far (as) amesema: "Taqiya ni kwa kila dhara na mwenye kufanya taqiya ndio anajua zaidi pale inapompata."

"Na sharti la madhara na kudhurika katika mfano wa habari hii halipingi taqiya kuthibiti katika sehemu zisizo na madhara kama vile sehemu za uelewano na nyinginezo kama ilivyotangulia, hiyo ni kwa ujumla wa hoja hizo zenye kujumuisha sehemu za uelewano na upendo ambazo hazikubali kuzingirwa na madhara, kwa sababu uelewano na upendo ni jambo moja na madhara na kudhurika ni jambo jingine, vivyo hivyo hakuna mpaka wa upendo na uelewano unazoziwajibisha, nao vile vile unatizama hali halisi na unatofautiana kwa kutofautiana wakati, sehemu, watu na ada.

"Kuanzishwa taqiya ni kwa ajili ya kuondoa ikhtilafu na kuleta umoja, uelewano, wepesi na kuleta neema kwa watu, na yote haya yanapelekea sala kusihi na kutosheleza katika sehemu zote za taqiya bila ya kuwepo haja ya kurudia wala kulipa kadhaa. Kwa sababu kuwajibisha kurudia na kulipa kadhaa ni miongoni mwa vitu vinavyopelekea kukimbiana na kuchukiana, na haya yanapingana na hekima ya kuruhusiwa kwake. Yote hayo yanathibitishwa na ujumla wa hoja za taqiya na upana wake, na habari ni nyingi zinazoraghibisha hilo kwa kauli mbali mbali. Madhumuni ya ujumla uliopokewa katika taqiya ni kwamba uhalali wake hauna sharti la kutokuwa na ujanja wa kujitetea…."[1]

Katika maelezo ya kufafanua maana ya taqiya katika mafunzo ya Alhul-Bait (as) mtafiti Ustadh wa masomo ya juu katika Hawza ya Kielimu Sheikh Ahmad Abidiyn amesema: "Taqiya sio kwa ajili ya hofu ya kuuliwa, kupigwa au kwa yasiyokuwa hayo miongoni mwa madhara ya kimwili tu, bali wakati mwingine inakuwa ni kwa ajili ya kuhifadhi dini na Umoja wa Waislam, kwa ajili hiyo ndio maana tunaona katika riwaya kwamba sehemu tisa kati ya kumi (9/10) za dini zipo katika taqiya, na kwamba hakuna dini kwa asiyekuwa na taqiya.

[1] *Muhadhabul-Ahkam* Juz. 2, Uk. 384 -389 chapa ya IV ya mwaka 1413 A.H chapa ya Muasastu al Manaar- Qum

"Mtafiti yeyote mwenye kuchunguza katika hadithi hizi ataona kwamba maelezo haya hayaafikiani na suala la kuhifadhi nafsi kutokana na dhalim au mtawala mwovu, wala hakuna yeyote anayesema kwamba Yasir na Sumayah wazazi wa Ammar hawana dini, kwa sababu wao waliacha taqiya, au Zaid bin Ali bin Husein hana dini kwa sababu aliacha taqiya, au wale waliokwenda katika ziara ya Imam Husein (a.s.) kisha wakafa shahidi katika njia yake katika zama ya Al-Mutawal al- Abbasiy hawana dini kwa sababu waliacha taqiya. Bali Hadith hizi zinaafikiana na hali ya mwenye kuacha taqiya na kitendo chake hiki kikawajibisha kufarakanisha safu za Waislamu au kusababisha makafiri kuteka nchi ya Kiislam au kudhoofisha na kuporomosha utamaduni na uchumi.

"Maimamu wetu (as) ambapo walikuwa wanaona masaibu haya waliafikiana juu ya jambo la taqiya na kulifanyia kazi, hivyo walihudhuria katika swala za Ahlus-Sunna, walitembelea wagonjwa wao, waliswalia majeneza yao na waliwaamuru Mashia wao juu ya hilo na kwa kauli moja: 'Maimamu walisisitiza kuunganisha neno ili neno la umoja libaki hai.'

"Kidogo kidogo lengo la taqiya likabadilika kutoka katika kuhifadhi dini na kwenda kwenye kuhifadhi nafsi na likaingia katika vitabu vya fiqhi vilivyokuja baadae na kuwa ni mwenza  wa dharura, licha ya kwamba dharura na taqiya ni anwani mbili ambazo kila moja yajitegemea. Dharura ni hukumu ya pili kwa ajili ya kuhifadhi nafsi dhidi ya kuhiliki, hukumu ambayo inaenea katika kila kitu, ama taqiya yenyewe imewekwa kwa ajili ya kuhifadhi dini."[1]

## Fatwa ya Imam Khomeni:

Katika mwanzo wa msimu wa Hijja baada ya ushindi wa  Mapinduzi ya Kiislamu ya Iran chini ya uongozi wa Imam Khomeni (r.a.) mwaka 1409 A.H. alitoa tangazo kwa mahujaji wa kiiran na kwa mashia wote tarehe 28 Shawwal 1399 A.H. Katika hotuba hiyo aliwataka kushiriki katika swala ya jamaa pamoja na Ahlus-Sunna na kujiepusha na kitendo chochote kinacholeta mtengano na mfarakano baina ya Sunni na Shia. Katika tangazo hilo alisema: "Inalazimu kwa ndugu zangu Wairan na Mashia wote kutoka katika nchi za Kiislaam kujiepusha na vitendo vyote viovu vinavyosababisha mfarakano katika safu za Waislam, na inalazimu kuhudhuria katika jamaa za Ahlus-Sunna na kujiepusha kabisa kuswali swala ya jamaa majumbani na kuweka vipaza sauti katika njia zisizozoeleka, na kujitupa juu ya makaburi matakatifu na kujiepusha na vitendo ambavyo vinaweza kukhalifu sheria."[2]

Na tangazo la Imam Khomeni lilikuwa na athari ya kivitendo ambapo mahujaji wa Kiirani walishikamana na wito huo na wakapokelewa rasmi na pande zote za kidini katika mamlaka ya Saudi Arabia kwa furaha na heshima.

---

[1] Aabadiy: Sheikh Ahmad  katika *Al –Wahdatul- Islamiyau Baina shiaari Wal-Amali, MajalatunususiL-Mu'aswirati* Adad 11 swaif 2007 Markazul-Buhuthil-Muaswirat – Beirut.

[2] Suhaaniy: Ja'far katika Da*uru Shiati Fiy Binail-Hadharatil Islamiyah* Uk: 10 chapa ya pili ya Muawiniyatu shuuni taaliymwal buhuthul Islamiyah  - Iran.

Fatwa ya Imam Khomeni haikuishia katika kuswali pamoja na Ahlus-Sunna katika sehemu ya Hija tu, bali aliulizwa swali: "Je, inawezekana kwa Shia kufuata swala ya jamaa kwa imam wa Kisunni katika sehemu isiyokuwa ya Hija au laa?" Akajibu: "Wanaweza kufanya hivyo."[1]

Na aliulizwa swali lifuatalo: "Kufuatana na fatwa ya Imam, ni sharti imam wa jamaa awe Shia, baadhi ya wanafunzi wa Kiirani wanaosoma vyuo vikuu nje ya nchi kulingana na fatwa hii hawashiriki katika misikiti na jamaa ya Waislam, na kitendo hiki kinaleta mtazamo mbaya kwetu kwa Waislam wengine. Je, kitendo hiki ni sawa kisheria au hapana?" Akajibu: "Ikiwa kutoshiriki swala pamoja na hawa kunaleta picha mbaya, basi shirikini na salini pamoja nao.[2]

**Fatwa ya Sayyid Khuiy:**

Sayyid Khuiy (1317 A.H. / 1413 A.H.) ambaye ni kati ya Marja'a wakubwa wa Kishia, alijibu mengi kati ya mas'ala ambayo yanahusu kusihi kwa swala ikiwa utasali pamoja na Ahlus-Sunna katika jamaa. Alisisitiza katika moja ya majibu yake kwamba ni mustahabu kuswali nyuma ya imam wa Kisunni, na kwamba hiyo haihusu tu wakati wa hofu wala dharura. Alipoulizwa swali lifuatalo: "Je, kuswali nyuma ya imam asiyekuwa Shia ni mustahabu, na ni vipi?" Akajibu: "Ndio ni mustahabu, na atasoma yaliyo wajibu kwake binafsi kimoyo moyo na hakuna ubaya yeye kumaliza kabla ya Imam, hapo atasubiri na atarukuu pamoja naye, na atasoma kimoyomoyo katika visomo vyake vyote, na wala hakuna sharti lolote isipokuwa ni kule tu (imamu) kuwa kwake mwislam asiyekuwa Shia. Imamu akiwa si Shia si lazima afungwe na masharti yote yaliyotajwa katika hali ya taqiya.[3]

Kama ambavyo Sayyid Khuiy ametoa fatwa juu ya kuhudhuria swala ya jamaa ya Ahlus-Sunna katika sehemu ambazo swala ya jamaa ya Kishia haipatikani, hiyo ni alipoulizwa swali lifuatalo: "Je, inajuzu waumini kumfuata imam asiyekuwa Shia katika ijumaa na jamaa pale ambapo haipatikani ijumaa wala jamaa ya Kishia?" Akajibu: "Ndio inajuzu kumfuata ila mwenye kufuata atasoma mwenyewe na wakati huo haitompasa kurudia, haya ni katika yasiyokuwa ijumaa. Ama kuhusu ijumaa haitatosheleza Adhuhuri."[4]

Na alipoulizwa juu ya sharti la uadilifu je, inalazimu litimie kwa imam wa Kisunni ili kuswali nyuma yake kama ambavyo ni sharti kutimia kwa imam wa Kishia? Akajibu: "Uadilifu hauzingatiwi katika swala hili."[5]

---

[1] Khomeni: Sayyid Ruhullah Al-Musawiy katika *Ahkamul-Islami Baina Saailu Wal–Imam*, mas'ala ya 484 uk: 223

[2] Khomeni: Sayyid Ruhullah Al Musawiy katika *Ahkamul-Islami Baina Saailu Wal–Imam*, mas'ala ya 482 Uk. 222.

[3] Khuiy: Sayyid Abul-Qasim katika *Swiratun-Najaat* Juz.1, Uk. 102, mas'ala ya 257, Chapa ya 2, ya 1416 A.H ya Maktabatul-fiqihiya - Kuwait.

[4] Khuiy: Sayyid Abul-Qasim katika *Swiratun-Najaat* Juz.1, Uk. 101, mas'ala ya 255, Chapa ya 2, ya 1416 A.H ya Maktabatul-fiqihiya - Kuwait.

[5] Khuiy: Sayyid Abul-Qasim katika *Swiratun-Najaat* Juz.1, Uk. 102, mas'ala ya 256, Chapa ya 2 ya 1416 A.H ya Maktabatul-fiqihiya - Kuwait.

Sayyid Khuiy ameashiria katika sehemu zinazofaa Shia kuswali pamoja na ndugu zao Masunni, na zinazoonekana zaidi ni kudhihirisha umoja katika safu za umma. Ambapo aliulizwa: "Nini falsafa ya kuswali jamaa pamoja na ndugu zetu masunni?"' Akajibu: "Kati ya hizo ni kudhihirisha umoja katika safu za Waislam."

Na Sayyid Khuiy anaona kwamba katika kuswali swala ya jamaa pamoja na Ahlus-Sunna ni lazima kuzingatiwa humo hukumu zote za swala ya jamaa ya Kishia isipokuwa kusoma. Na swali lililoulizwa lilikuwa ni hili: "Je, mtu akiswali jamaa pamoja na Sunni hukumu zote za swala ya jamaa zinazingatiwa kama ilivyo katika jamaa ya Shia, kama vile kurejea kwa imam anayekumbuka wakati wa shaka katika idadi ya rakaa, au kama vile kusamehewa kuzidisha rukuu atakaposimama kabla ya imam kwa kusahau, hivyo anarejea ili kumfuata?" Jibu lake lilikuwa kama ifuatavyo: "Ndio, zinazingatiwa hukumu zote isipokuwa kisomo, kwani imam hambebei, hivyo ni lazima asome mwenyewe.[1]"

## Fatwa za Sayyid Sistaniy:

Sayyid Sistaniy naye ndiye Marja'a mkuu wa Kishia leo, alipinga baadhi ya Shia kutoka katika Misikiti miwili Mitakatifu, Makka na Madina wakati inapokimiwa swala ya jamaa, ambapo aliuzwa swali lifuatalo: "Tunaona baadhi ya Waumini wanatoka inapokimiwa swala katika Misikiti miwili Mitakatifu, nini maoni yenu?" Akajibu: "Kitendo hiki sio kizuri, bali haijuzu kwani kinaleta sura mbaya kwa Madhehebu."[2]
Na alipoulizwa kuhusu kuswali jamaa katika mahoteli huko Makka na Madina kwa baadhi ya mahujaji na wenye kufanya ziara. Akajibu kwamba ni bora kushiriki swala ya jamaa katika Misikiti miwili Mitakatifu kwa lengo la kuleta uelewano baina yao."[3]

## Fatwa ya Sayyid Khameneiy:

Sayyid Khameneiy Kiongozi Mkuu wa Mapinduzi ya Kiislamu ya Irani aliulizwa: "Je, inajuzu kuswali swala ya jamaa nyuma ya Sunni"? Akajibu: "Swala ya jamaa ni kwa ajili ya kuhifadhi Umoja wa Waislam, inajuzu na ni sahihi."[4]

Na alipelekewa swali lifuatalo: "Sehemu yangu ya kazi ipo kwa Wakurdi, na maimamu wao wengi wa ijumaa na jamaa huko ni katika Ahlus-Sunna, nini hukumu katika kuwafuata?" Akajibu: "Hakuna mushikeli katika kushiriki swala pamoja nao katika ijumaa zao na jamaa zao kwa ajili ya kuhifadhi Umoja wa Kiislam."[5]

---

[1] Khuiy: Sayyid Abul-Qasim katika *Swiratun-Najaat* Juz. 3, Uk. 74, mas'ala ya 214, Chapa ya 2, ya 1416 A.H ya Maktabatul-fiqihiya- Kuwait.
[2] Sistaniy: Sayyid Ali Huseiniy katika *Mulhaq Manasikil-Haji* Uk. 455, chapa 1, ya 1426 A.H, ya Maktab Sayyid Sistaniy - Qum
[3] Sistaniy: Sayyid Ali Huseiniy katika *Mulhaq Manasikil-Haji* Uk. 455, chapa 1, ya 1426 A.H, ya Maktab Sayyid Sistaniy- Qum
[4] Khameneiy: Sayyid Ali Al–Huseiniy katika *Ajwibatul-Istiftaati*, Mas'ala ya 598, chapa 1 ya 1420 A.H Mashuraat Karbalaai - Iraq.
[5] Khameneiy: Sayyid Ali Al–Huseiniy katika *Ajwibatul-Istiftaati*, Mas'ala ya 599, chapa 1 ya 1420 A.H Mashuraat Karbalaai - Iraq.

Hapa utaona kwamba swali linahusu sehemu katika nchi ya Irani yenye serekali, na wengi wao ni Shia, pamoja na hivyo Kiongozi wake mwanachuoni anaelekeza kushiriki katika swala ya jamaa ya wachache ambao ni Sunni.

Aliulizwa swali lifuatalo: "Nini hukumu ya kushiriki katika swala ya jamaa ambayo inaswaliwa katika nchi za Ulaya na nyinginezo na wanafunzi wa vyuo vikuu ambao ni wa nchi za Kiislam na ambao wengi wa wanaoshiriki humo na hali imam ni kati ya Masunni? Je, katika hali hii inalazimu kuswali swala ya Adhuhuri baada ya swala ya Ijumaa?" Akajibu: "Hakuna ubaya kushiriki humo kwa ajili ya kuhifadhi umoja na mshikamano wa Waislam na wala sio wajibu kuswali swala ya Adhuhuri baada ya swala ya Ijumaa."[1]

Na ni kama ambavyo aliulizwa swali lifuatalo: "Misafara ya kidini kutoka sehemu za Qatifu na al-Ahsai inatoka kwa ajili ya kuzuru sehemu takatifu Makka na Madina, na misafara hii inaswali swala ya jamaa mahotelini, je hiyo inajuzu? Na nini hukumu ya swala ya furada hotelini? Je, ni wajibu kushiriki swala ya jamaa katika Haram Tukufu?" Akajibu: "Inapasa kwa waumini katika msimu wa Hijja katika Madina na Makka Tukufu ambapo ni mahali pa kuhudhuria wageni kutoka makundi yote ya Kiislam na nchi zote, wazingatie Umoja wa Kiislam kwa kushiriki pamoja na Waislam wengine kuhudhuria katika misikiti na kuswali pamoja nao katika jamaa, na wala wasizoee kuswali mahotelini na majumbani hata kama ni kwa kuswali furada, na hii ni ikiwa kuswali jamaa majumbani na hotelini hakutakuwa ni kinyume na maslahi ya Uislam na Waislam, vinginevyo haijuzu (kusali mahotelini na majumbani)."

Na aliulizwa swali lifuatalo: "Baadhi ya Waumini wanatoka inapokaribia adhana katika Haram Tukufu au wanakwenda katika Haram punde tu, baada ya kumalizika swala, nini maoni yenu juu ya hilo?" Akajibu: Haijuzu kutoka katika safu za jamaa na katika Haram Tukufu ya Madina au Makka wakati wa swala ya jamaa au inapokaribia kusimamishwa swala ya jamaa, bali ni wajibu wakati huo kushiriki pamoja nao katika swala yao. Ama kwenda katika Haram na kuingia Msikitini baada ya kumalizika swala ya jamaa katika Haram hakuna kizuizi maadam haidhihirishi kutojali swala yao, kama kuingia Haram itakuwa ni kwa ajili ya mkusanyiko."[2]

### Fatwa ya Sheikh Husein Al-Usufur:

Ametia mkazo Al-Faqih Sheikh Husein Al-Usufur (aliyefariki mwaka 1216 A.H) katika kitabu chake *Sadadul-Ibaad* juu ya kupendeza kuhudhuria swala ya jamaa pamoja na wale anaotofautiana nao katika madhehebu, hata kama atakuwa ameshaswali faradhi yake. Hivyo ni mustahabu kwake kushiriki nao vile vile. Na Kujuzu kushiriki pamoja nao haihusiani na hali ya dharura tu, bali hata pasipo na dharura. Amesema katika mas'la ya 11 katika mambo yanayohusu swala ya jamaa: "Umeshatangulia uhakiki wa yale ambayo yanapelekea iwe ni mustalabu kuhudhuria jamaa ya wasiokuwa sisi wale tunaotofatiana

---

[1] Khameneiy: Sayyid Ali Al-Huseiniy katika *Ajwibatul-Istiftaati*, Mas'ala ya 620, chapa 1 ya 1420 A.H ashuraat Karbalaai - Iraq.
[2] www.raoofonline.com

nao, na kwamba ni sunna yenye nguvu kiasi kwamba mwenye kuswali pamoja nao katika safu ya kwanza ni kama vile mwenye kuswali nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) katika safu ya kwanza. Na hayo ni sawa awe amesali faradhi peke yake au hajaswali. Na mwenye kuswali furada kisha akahudhuria akaswali nao basi atapata malipo ya mema yao. Na wala sio sharti katika kujuzu kuswali pamoja nao kutokuwepo jinsi ya kuwakwepa, inajuzu bila hata ya dharura."[1]

Na kutokuwa na dharura, yaani kutokuwa na wasaa, kwa maana ya kwamba kujuzu kuswali katika jamaa ya Ahls-Sunna sio kwa sharti la dharura na kutokuwa na namna ya kujinasua bali inajuzu hata bila ya kuwa na dharura.

## RAI YA SHARIA NA UHALISIA WA KIJAMII

Kama ilivyotangulia kueleza hakika kila kundi kati ya Waislamu Sunni na Shia wana misikiti yao na swala zao za jamaa kulingana na masharti ya kusihi uimam wa jamaa kwa kila makundi mawili. Na ni kawaida kwa wafuasi wa kila madhehebu kwenda katika misikiti yao na kuswali swala zao kulingana na hukumu za madhehebu yao. Lakini mazungumzo ni juu ya sehemu za mikutano na mikusanyiko, na kati ya hizo ni hizi zifuatazo:-

Katika Haram mbili Tukufu wakati Shia wanapokwenda kutekeleza Hija na Umra. Katika ofisi na taasisi ambapo humo wanafanyakazi baadhi ya Mashia, na ndugu zao Masunni wanasimamisha swala ya jamaa. Katika mikutano na makongamano ambapo humo kuna washiriki wa madhehebu mbali mbali. Katika safari na kusindikizana na wakati wanapokutana watu wa pande mbili. Katika sehemu kama hizi rai kisharia ya madhehebu ya Ahlul-Bait iko wazi kupitia nasi zilizopokewa kutoka kwa Maimam (as) na kupitia sira yao na maelezo ya rai zao, na kupitia fatwa za maulamaa wa Kishia. Hakika kinachotakikana kwa Mashia katika mfano wa sehemu kama hizi ni kushiriki katika swala ya jamaa na ndugu zao Masunni kwa ajili ya kuimarisha uelewano, umoja na ukuruba.

Na kama tukichukulia kimazingatio mazingira yaliyopo sasa ambayo umma unaishi nayo, hakika ushiriki huu utaonekana kuwa una umuhimu mkubwa na unahitajika sana. Kwa sababu kuna anayetaka kuchochea fitina za kimadhehebu na kuna ambaye anahamasisha na kuchochea chuki baina ya pande mbili, na kuna propaganda ovu na matangazo ya upotoshaji yanayowaelezea Shia na madhehebu yao kwa sura mbaya mbele ya Waislam wengine. Na kama Shia watajiondoa katika kuswali pamoja na ndugu zao Masunni katika sehemu kama hizi, basi watatoa fursa ya kufaulu majaribio hayo yenye kuleta sura mbaya baina yao na baina ya Waislamu wengine, na hivyo kuimarisha hali ya mfarakano na mgawanyiko. Wakati ambapo kushiriki kwao katika swala ya jamaa ni kuvunja vikwazo vya kinafsi na kuondoa tuhuma batili na kutoa fursa ya kufahamiana na kuelewana.

---

[1] Aal Usfur: Sheikh Husain/ *Sadadul-Ibad* Juz. 1, Uk. 150.

Hakika Hijja na Umra ni kati ya fursa bora za kufahamiana na kuelewana baina ya Waislam ambapo Waislam wanawasili kutoka nchi mbalimbali na kutekeleza swala katika Haram mbili Tukufu, na huu ni mkusanykiko wa kawaida kwa hawa Mahujaji na wenye kufanya Umra, hivyo Shia wanaposambaa ndani ya ndugu zao wengine wa Kiislam wakati wa swala wanapata fursa ya kujitambulisha na kuwatambua ndugu zao Waislam wa madhehebu na makundi mengine. Lakini wanapojitenga na swala yao katika sehemu za makazi yao basi wanakuwa wamepoteza kwa ajili ya nafsi zao fursa hiyo tukufu na wanapoteza manufaa kati ya manufaa muhumu ya Hijja na Ziara katika sehemu takatifu.

Vivyo hivyo hali ni hiyo katika sehemu za idara za kazi na asasi ambazo humo wanafanya kazi baadhi ya wafanyakazi Mashia, hakika kuhudhuria kwao katika swala ya jamaa pamoja na ndugu zao Masunni pale inaposimamishwa inatia mkazo kwamba wao ni sehemu katika jamii, na kwamba kuna uhusiano na kiungo kinachowaunganisha baina yao, wakati ambapo kujibagua na swala ya jamaa ni jambo linaloleta mfarakano wa ikhitilafu na kutoa mwanya wa tafsiri mbalimbali mbaya katika upande wao. Pamoja na kuwepo rai ya kisheria inayotoa msukumo wa ushirikiano na uwazi wa maslahi mahususi na ya kawaida katika hayo, ila baadhi ya Shia wanasitasita na kuwa na kigugumizi katka jambo hili. Na kati ya uadilifu na insafu ni kuashiria baadhi ya vyanzo na sababu za mandhari haya:-

**Kwanza:** Ni ile hali waliyoizoea watu wa kila upande kuwa na misikiti yao na swala yao ya jamaa, hali hiyo imejenga katika akili za watu dhana ya kutosihi ushirikiano. Pia kuna uzembe kutoka kwa Maulamaa na makhatibu katika kuwabainisha Mashia wa kawaida rai ya kisharia. Hivyo uongozi wa kidini wa Irani unapokuja na msimamo huu na kuupeleka katika Hijja, na kusambaza matangazo na fatwa na kuzuia misafari ya Hijja ya Kiirani kuswali swala ya jamaa katika mahoteli yao, Mashia wa Kiiran wamekuwa ni wenye kuitikia kwa wingi wito wa kushiriki katika swala ya jamaa katika Haram mbili Tukufu.

**Pili:** Kuweka sharti la kupatikana uadilifu kwa imam katika fiqhi ya Kishia na ambayo inasababisha Shia kuacha kuswali nyuma ya imam asiyemjua na asiye na matumaini ya uadilifu wake, baadhi ya Shia wamechupa mpaka katika kujilazimisha na sharti hili zaidi kuliko inavyotakikana kisheria. Hivyo wanaacha kushiriki katika swala ya jamaa pamoja na imam wa Kishia ikiwa hawamjui au pale wanapokosa matumanini na uadilifu wake. Lakini sharti hili halipo katika kuswali katika jamaa ya Ahlus-Suna, na haya ni ambayo wengi wa Mashia hawalijui au hawalitazami.

**Tatu:** Mazingira ya mashambulizi ya kimadhehebu dhidi ya Shia, yale yanayosababisha hali ya kulipiza kisasi, kwani Shia anaposwali nyuma ya imam wa Kisunni husikia katika hotuba yake maneno makali yakielekezwa kwao ikiwa ni kuwatuhumu katika dini yao na kuwaelezea kwa sifa batili, hivyo wanajiepusha kuswali jamaa ili kuziepusha nafsi zao na machungu ya kusikiliza uzushi huo. Hivyo ni wajibu kwa anayewaongoza Waislam na kuwahutubia hususan katika sehemu takatifu na sehemu zenye mchanganyiko ajilazimishe kutoa hotuba za Umoja wa Kiislam na alinganie mshikamano na uelewano kati ya

umma, na wala haisihi kwake kushangilia mfarakano na ikhitilafu na kuchochea chuki na bughudha baina ya Waislam.

**Nne:** Kuwepo hofu kwa baadhi ya Shia kwamba kuswali swala yao pamoja na Ahlus-Sunna kutachukuliwa kuwa ni aina ya udhaifu, woga na ni kutumia taqiya, na hii ni dhana isio sahihi. Ikiwa kuna Ahlus-Sunna wenye kuangalia jambo hili kwa sura hii basi ni kundi dogo sana ambalo limeathirika kwa propaganda na wanaweza kubadili mtazamo wao watakapoona ushirikiano wa Shia unaonekana na kuzoeleka.

Pia kuna hofu nyingine kwa baadhi ya Shia, nayo ni hofu juu ya watoto wao kuathirika kwa kuhudhuria kwao katika mazingira ya kidini ya Ahlus-Sunna, ambapo inaweza kudhoofisha mapenzi yao na ufuasi wao wa kimadhehebu. Kwa hawa wenye hofu tunasema hakika sisi hatuwalinganii watoto wa Kishia kuacha misikiti yao na kuswali katika jamaa yao, tumeshataja kwamba kati ya masharti ya kusihi uimam ni imam kuwa Shia Ithna Asharia, na tumeashiria kwamba ni kawaida na ni haki kila madhehebu kusimamisha swala ya jamaa kulingana na kanuni za madhehebu ambayo wanayafuata. Lakini mazungumzo ni katika sehemu za mkusanyiko na ambazo panaswaliwa swala ya jamaa. Kisha je hawa wenye woga wao huu ni wenye kujali Ushia zaidi kuliko Maimam wao na Marja'a wao?

Hakika kuimarisha ufuasi wa madhehebu kunakuwa kwa malezi mema na ufahamu sahihi na wala sio kwa kujitenga na kujibagua, jambo ambalo ndio kimbilio la madhaifu wasiojiamini na wasiojikinaisha.

## HUKUMU ZA KUSWALI JAMAA PAMOJA NA AHLUS-SUNNA

1. Kongamano la Maulamaa wa Kishia wameafikiana juu ya kupendeza kuswali swala ya jamaa pamoja na Ahlus-Sunna kwa ajili ya kuhifadhi umoja na kuleta uelewano na mshikamamo. Sayyid Al-Mar'ashiy amelihesabu kuwa ni kati ya kongamano la fiqhi ya Kishia, amesema: "Hakuna kuswali nyuma ya wenye kuchupa mipaka katika kusifu, lakini ni ruhusa kuswali nyuma ya unayetofautiana naye katika madhehebu kama italazimika kutumia taqiya au maslahi ya jumla, na kwa ajili ya manufaa ya umma, kwa ajili ya kuleta umoja na kupata nguvu dhidi ya maadui.[1]

2. Sio sharti kwa imam wa jamaa ya Ahlus-Sunna kutimiza lolote kati ya masharti ya kusihi uimam yaliyotajwa katika fiqhi ya Kishia.

3. Ikiwa kuacha kuswali pamoja na Ahlus-Sunna inawajibisha udhalili kwa Uislam au kuleta sura mbaya kwa madhehebu basi itakuwa ni haramu.

[1] Mar'ashiy: Sayyid Ismail bin Ahmad Al Huseiniy katika *Ijmaiyaatul-Fiqhi Shiah* Juz.. 1, Uk. 486 chapa ya 2 ya 1998

4. Sunni wote wanasoma nyuma ya imam, ima kwa kuwa ni wajibu kama asemavyo Imam Shafiy, na ima ni kwa kuwa ni mustahabu katika swala za kuficha na ni makruhu katika swala za kudhihirisha, isipokuwa kama atakusudia kuheshimu tofauti hapo itakuwa ni mustahabu hata katika swala za kudhihirisha, hiyo ni kulingana na rai ya Malikia. Na Hanbali wanaona kwamba ni mustahabu kusoma nyuma ya imam katika swala za kuficha, na pale imamu anaponyamaza katika swala ya kudhihirisha, na ni makruhu wakati anaposoma imam katika swala ya kudhihirisha. Ama Hanafi wao wanaona kuwa maamuma kusoma nyuma ya imam ni makruhu bali ni haramu.[1]

Baadhi ya Maulamaa wa Kishia kama vile Sayyid Khuiy, Sayyid Sistaniy, Sayyid Shiraziy na wengineo wanaona kwamba Shia anaposwali pamoja na Ahlus-Sunna ni juu yake kusoma katika rakaa mbili za kwanza, Sura ya Al- Hamdu na Sura nyingine kati ya Sura fupi, na kusoma kwake kuwe kimya kimya hata kama itakuwa ni katika swala zilizo wajibu kudhihirisha. Na ikiwa imam amerukuu na wakati ukawa haukutosha kusoma Sura basi inatosha kusoma Al- Hamdu, na ikiwa atamaliza kusoma kabla ya imam basi atashughulika kwa kusoma tasbihaati. Wakati ambapo baadhi ya maulamaa wanatoa fatwa ya kutolazimika kusoma, na hayo yanadhihirika katika fatwa ya Imam Khomeini, Sayyid Khameneiy, Sheikh Fadhil Al-Ankaraaniy, Sheikh Nasir Makarim As-Shiraziy na Sheikh Yusuf As-Swana'aniy.

Imekuja katika fatwa ya Skeikh Al-Ankaraaniy kwamba: "Kuswali nyuma yao inakuwa kwa nia ya jamaa, na wala sio wajibu humo kusoma yeye binafsi, na inakuwa sahihi na haihitaji kulipa kadha au kurudia."

Na Sheikh Makarim Shiraziy anasema: "Ni dhahiri katika jumla ya riwaya za Ma'asumina kwamba akusudie kumfuata imam na atende kulingana na naye bila ya kuwepo na haja ya kuirejea au kusoma Al-Hamdu na Sura."

Sheikh Swana'aniy anasema: "Kushirikiana pamoja nao katika swala ya jamaa ni kama vile kushiriki katika jamaa pamoja na imam wa Kishia, hivyo swala ya jamaa pamoja nao inakuwa kwa nia ya kumfuata imam, na kusoma kunaporomoka kwa mwenye kuswali, na yanampasa yote yanayompasa maamuma, na vipi isiwe hivyo wakati swala ya jamaa ina mengi ikiwemo kuhifadhi umoja, utukufu wa swala ya jamaa na uelewano baina ya Waislam ambao umeamrishwa katika Sheria kwa msisitizo.

5. Shia ataswali swala yake pamoja na Ahlus-Sunna kulingana na hukumu za swala katika madhehebu ya Shia, hivyo atanyoosha mikono yake na wala hataifunga, na kunyoosha mikono na kutoifunga ni sunna kwa baadhi ya Sunni, nao ni Mamalikia. Wala asiseme Amin baada ya imam kumaliza kusoma Al-Hamdu, wala asisujudu juu ya yale yasiyosihi kusujudu juu yake. Lakini kujilazimisha kwa chochote kati ya hukumu hizi ikiwa kutasababisha mushkeli au kuleta madhara

[1] *Al-Mausuatul Fiqihiyah* Juz. 33, Uk. 52- 53 chapa ya 1, ya 1992 Wizaratul Auqaaf wa Shuunil- Islamiyah – Kuwait.

basi haitakuwa ni wajibu, inajuzu kwa Shia kufunga mikono na kusujudu juu ya busati kwa ajili ya kuzuia madhara yanayotarajiwa, na swala yake itakuwa sahihi na wala haihitaji kuirudia. Ama kunuti kabla ya rukuu ya pili ni sunna na wala kuicha haileti kasoro katika swala na inawezekana kuileta bila ya kunyanyua mikono, bali itatosha kwa dua kama wakati utatosha kabla ya rukuu ya imam.

6. Hakuna tofauti katika wakati wa swala baina ya Shia na Sunni isipokuwa swala ya magharibi ambapo Shia wanaichelewesha hadi uondoke wekundu wa Mashariki, yaani kiasi cha dakika kumi baada ya kuzama jua ambapo kwa Ahlus-Sunna ni kuiwahisha swala ya jamaa kwa mfano wa kiasi hiki, hivyo kwao haisimamishwi jamaa misikiti punde tu baada ya kuingia wakati. Hivyo hakuna mushkeli kuswali pamoja na Ahlus-Sunna katika yale yanayohusiana na wakati, isipokuwa yale tuliyoyaashiria katika swala ya magharibi, kwani inasihi kuswali pamoja nao pale wanapoichelewesha kwa kiasi cha dakika kumi.

7. Ikiwa Shia ameshaswali na ikasimamishwa swala kwa Ahlus-Sunna ni sunna kuswali pamoja nao kadhaa kwa yale ambayo yanaweza kuwa katika dhima yake miongoni mwa swala zilizopita.

## NASAHA NA MAELEZO

Kufuatana na maelekezo ya maimam wa Ahul-Bait (as) na majibu ya fatwa za maulamaa na Marja'a na kwa ajili ya kuimarisha Umoja wa Kiislam na wa nchi, na kupoteza fursa kwa mwenye kuchochea fitina za makundi na fotauti za kimadhehebu, nawalingania ndugu zangu Mashia kushiriki katika swala ya jamaa pamoja na ndugu zao Masuni katika sehemu za mikusanyiko na mijumuiko kama vile msimu wa Hijja na Umra, kwa kujali swala ya jamaa katika sehemu mbili takatifu. Kama ambavyo nawausia wafanyakazi Mashia kushiriki swala ya jamaa ambayo inaswaliwa katika sehemu zao za kazi, pia nawausia wanangu wanafunzi wa vyuo vikuu kuswali swala ya jamaa inayoswaliwa katika vyuo vyao. Na haipaswi kwa yeyote kuswali swala ya furada katika sehemu ambayo humo inaswaliwa swala ya jamaa ya Ahlus-Sunna.

Baadhi wanaweza kutoa kisingizio cha kutokushiriki swala ya jamaa kwa Ahlus-Sunna kwa kuogopa kutazamwa vibaya na baadhi, ya kwamba wao wanajipendekeza na kwamba wanafanya taqiya. Lakini hii ni tuhuma tu, kama wapo wenye kufasiri mambo kihivyo basi hao ni wachache kati ya wenye msimamo mkali na haipasi kukhalifu rai ya kisheria na kukosa thawabu na maslahi yanayotarajiwa kwa sababu yao.

Hakika hali halisi ya uzoefu inaonyesha kwamba Ahlus-Sunna hufurahia kitendo cha Shia kuswali pamoja nao kwa kuwepo athari nzuri ambayo inaletwa na ushirikiano na uhusiano baina ya pande mbili, ama yule anayetazama hilo kwa mtazamo mbaya miongoni mwa Ahlus-Sunna, yawezekana atakuwa ameathirika kwa propaganda za uchochezi dhidi ya Shia au atakuwa ni mwenye kuchupa mipaka asiyependa uhusiano na utengamano baina ya Shia na Sunni.

Na ni juu yetu tusiwape hawa fursa ya kutekeleza maelekezo yao ya kiubaguzi yenye kuchukiza, bali tujilazimishe kufuata maelekezo ya Maimam wetu Watukufu (as) na tujali umoja na ushirikiano katika yale yanayoleta maslahi ya kidini na nchi. Mwisho wa ulingano wetu ni kwamba Shukrani zote njema anastahiki Mola Mlezi wa viumbe.

## BIBLIOGRAFIA


1. Ibnu Qudamash Al-Hambaly: Abdallah bin Ahmad katika Al-Mughuniy chapa II ya 1412 A.H, chapa ya Cairo.

2. Aal–Usufur: Sheikh Husein katika *Sadadil-Ibaad*, ya Majimaul–Buhuthil – Ilimiyah 1421 A.H - Chapa ya Qum.

3. Al-Burjurdy: Sayyid Husein Atabatabaiy katika *Jamiu Ahadiythus – Shiah*, Chapa I, 1417 A.H. Qum.

4. Al-Jaziriy: Sheikh Abdur-Rahman katika *Al-Fiqihil-Islamiy Alal–Madhahibil Arubaah* – Chapa ya Daru lhiyai Turath Araibiya- Beirut.

5. Al- Hurul-Aamily: Muhammad bin Hasan katika *Wasailus–Shiah*, Chapa I, 1993 ya Musasati Aal Al- Bait liihiyai Turath – Beirut.

6. Khameneiy: Sayyid Ali Huseiniy katika *Ajiwibatul-Istiftaati*, Chapa I, 1425 A.H Manshurat Karbalail Muqadasah – Iraq

7. Khomeni: Sayyid Ruhullah al –Musawiy katika *Ahkamul- Islami Baina Saail Wal-Imam*, Chapa I, 1993 – Darul- Wasilah – Beirut

8. Khuiy: Sayyid Abul-Qasim katika *Swiratun-Najaat*, chapa II, 1416 A.H Maktabatul-Fiqihi- Kuwait.

9. Azahiyl: Dokta Wabahah katika *Al-Fiqihil-Islamiy Waadilatihi*, Chapa III 1409 A.H – Damascus Darul- Fikri.

10. Subhaniy: Sheikh Ja'far katika *Dauru Shiati Fiy Binail-Hadharatil- Islamiyah*, Chapa II 1416 A.H Muawiniyati Shuuni Taalim Wal-Buhuthil-Islamiyah - Iran.

11. Asabzawary: Sayyid Abdul-Alla katika *Muhadhabul-Ahkam*, Chapa IV, 1413 A.H Muasasatil – Manaar - Qum

12. Sistaniy: Sayyid Ali Al-Huseiniy – *Mulhaqu Manasikul-Hajji*, Chapa I, 1426 A.H Maktab Sayyid Sistaniy – Qum.

13. Sistaniy: Sayyid Ali Al- Huseiniy –*Minhaajus-Swahilihiyna*, Chapa I, 1423H- Qum

14. Aabidiniy: Sheikh Ahmad katika *Al-Wahdatul-Islamiyat Baina Shi'ari Wal-Amal*, Jarida la kisasa, Toleo la 11, Swaif 2007/1428 A.H. Markazul- Buhuthil- Muaswirah - Beirut.

15. Marwariyd: Ali Asghar katika *Silsilatul-Yanabiy'il- fiQhiyah* –Swala, Chapa I, 1413 A.H Daru Turath – Beirut.

16. Al-'Anasiy As-Swana'aniy: Allammah Ahmad Qasim katika *Taajul–Madhhab Lil-Ahkaamil- Madhhab* - Maktabatul Yaman Al-Kubra – Sanaa.

17. Al-Mar'ashiy: Sayyid Ismail bin Ahmad Al- Huseiniy katika *Ijmaiyaati Fiqhi Shi'ah*, Chapa II, 1998.

18. *Mausu'atul-Imam* cha Sayyid Abdul-Huseiniy Sharafud-Diyn - Markzul-Ulumi Wathaatil-Islmiyah, Chapa I, 1427 A.H Darul- Muarikhil- Arabiy – Beirut.

19. *Al- Mausutul-Fiqhiyah*, Chapa I, 1992 Wizaratul-Awqaf Washuunil-Islamiyah-Kuwait.